

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



**MAADHIMISHO YA SIKU YA KIMATAIFA YA TEHAMA KWA WASICHANA
MWAKA 2021**



**KUTOKA KWA DKT. JABIRI K. BAKARI, MKURUGENZI MKUU WA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**KAULI MBIU: “WASICHANA WALIOUNGANISHWA, HUANDAA
MUSTAKABALI WAO”.**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na nchi nyingine duniani ambazo ni wanachama wa Shirika la Mawasiliano Duniani (International Telecommunication Union -ITU) katika huadhimisha siku ya kimataifa ya TEHAMA kwa Wasichana. Siku hii inaadhimishwa kila mwaka siku ya Alhamisi ya nne ya mwezi Aprili, ambapo kwa mwaka huu inaadhimishwa tarehe 22 Aprili, 2021 na maadhimisho hayo yakiwa yanafikisha miaka 10. Kauli mbiu katika maadhimisho hayo mwaka huu ni **“Wasichana waliounganishwa, huandaa mustakabali wao”**.

ITU ni shirika la Umoja wa Mataifa lililooundwa ili kusimamia mawasiliano kwa ujumla pamoja na mgawanyo wa masafa na kusimamia viwango vya vifaa vya mawasiliano ili kuhakikisha kuwa (TEHAMA) yanawafikia wananchi wote duniani bila kujali eneo la kijografia, Jinsia au hali ya kiuchumi.

Tunapoadhimisha siku hii, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekuwa ikiandaa shughuli mbalimbali zinazoshirikisha wadau kutoka kwenye sekta mbalimbali na hasa wale wanaotumia mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kuwapa elimu na uelewa Wasichana, na kuwahamasisha katika kupenda na kusoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhndisi na Hesabu.

Sambamba na kauli mbiu ya mwaka huu, TCRA inawajibika katika kuweka mazingira rafiki ya kuwawezesha Wasichana kutumia TEHAMA vema katika shughuli mbalimbali za masomo, kiuchumi na kijamii na hivyo kuwawekea msingi mzuri kwa maisha bora ya baadae.

TCRA katika kutekeleza majukumu yake ya kimkakati inasaidia miradi mbalimbali inayochochea ufikishaji wa huduma za mawasiliano, ikiwa ni pamoja na utoaji wa vifaa vya TEHAMA mashulen, zikiwemo shule mchanganyiko na zile za Wasichana na utoaji wa vifaa vya TEHAMA kwenye vituo vya TEHAMA vya jamii “Telecentres”. TCRA pia inaendesha programu za ushindani ambapo Wasichana hupewa kipaumbele kushiriki.

TCRA imetoea leseni kwa watoa huduma mbalimbali kwenye sekta ya mawasiliano ili kuwawezesha ufikishwaji wa mawasiliano katika sehemu mbalimbali nchini. Hii huwezesha vijana, ikiwa ni pamoja na Wasichana, kutumia mawasiliano ili kupunguza au kuondoa kabisa tabaka la upatikanaji wa huduma za TEHAMA na mawasiliano kwa ujumla.

Natoa wito kwa Wasichana hasa walioko shulenii waongeze bidii katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu; na kutumia vema TEHAMA kwenye shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi ili kujijengea msingi wa maisha bora ya baadae.

AHSANTENI